Ofisi ya Rais

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

MKOA WA ARUSHA S.L.P..43

Barua zote ziandikwe kwa Mkuu wa Shule MONDULI

Simu Na. +255 742930368 21/05/2018

Email: irkisongoss@gmail.com

Mzazi/ Mlezi wa…….. ……kidato cha Tano 2018.

YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018.

Uongozi wa Shule unayo furaha kukuarifu kuwa mwanao ……..... amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano (5) katika Shule ya Sekondari Irkisongo iliyopo Monduli Mjini Kaskazini mwa kituo cha mabasi monduli hatua 300 kutoka kituoni.“**Hongera sana na karibu mno”** Shule yetu ni ya wasichana tu kidato cha kwanza hadi cha sita.

SARE ZA SHULE

I.Sketi mbili **blue bahari (light blue)**zinapatikana shuleni kwa Tsh. 17,000 kila moja aje na fedha.
II. Shati mbili nyeupe Tetron mikono mirefu isiyobana mwili aje nayo.
III. Viatu vyeusi jozi mbili vya ngozi na sio vya ghorofa, vya kufunga kamba. Aje navyo.
IV. Sweta litapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/= aje na fedha.
V. Aje na Soksi ndefu nyeupe zinazofika kwenye magoti jozi mbili.
VI. Tai inapatikana shuleni kwa Tsh. 3,000/= aje na fedha.
VII. Picha 2 za paspoti (PPS) ya baba na mama au mlezi. Aje nazo.
VIII. Alete fedha ya kitambulisho sh. 7,000/=
IX. Aje na sh. 12,000/=kwaajili ya T-shirt yenye kola na nembo ya shule. .

VIFAA VYA DARASANI

-Madaftari makubwa 7 “COUNTER BOOK”QUIRE 3
-Madaftari madogo 7
-Mkebe “Mathematical Set”
-Kamusi ya Kiingereza (Oxford/Longman Dictionary)
-Kalamu za kutosha, rula na penseli
-Scientific calculator (CASIO fx-991MS) Kama anasoma EGM

VITABU

Kila mwanafunzi aje na vitabu vya mchepuo wake kwa kila somo kama ifuatavyo:-

1. **ECONOMICS**
   (i) Modern Economics by Robert Mudida
   (ii) Simplified Economics by N. A. Saleemi
2. **ADVANCED MATHEMATICS;**
   (i) Pure Mathematics 2 by J. K Backhouses
   (ii) Pure mathematics 1 by C.J Tranter
3. **GEOGRAPHY;**
   (i) Advanced level Practical Geography by Zist Kamili
   (ii) Human and Economic Geography by Msabila D. T.
   (iii) Physical Geography by Pritchard
4. **ENGLISH:**
   (i) Advance Level English by Asheli Nicholaus
   (ii) Advance Level Literature by Nyambari. N. & G.Bukagile
5. **KISWAHILI :**
   (i) Nadharia ya Lugha by Masebo & Nyambari N.
   (ii) Nadharia ya Fasihi by Nyambari N. & G. Bukagile
6. **HISTORY:**
   (i) Contemporary Historical Events Advanced level history 1& 2 by Mwl, Shibital C. K (ii) Advance Level History 2 by Oxford
7. **GENERAL STUDIES**
8. Understanding Advanced Level General Studies by Bigirwamungu J. And Deogratius S. M

SARE ZA KUVALIWA BAADA YA MASOMO

I. Sketi ya rangi ya kijani kikavu kwa tsh. 17,000/=inapatikana shuleni
II. Track suit ya kuvaliwa usiku nyeusi yenye mistari meupe pembeni aje nayo
III. T – Shirt ya rangi ya njano yenye kola isiyo na maandishi wala picha yoyote aje nayo
IV. Raba za kufunga kwa kamba na Bukta (kwa ajili ya michezo) aje nayo
V. Mabuti ya kuvaa wakati wa mvua na Mwamvuli mmoja aje nayo

VIFAA VINGINE ATAKAVYOLETA

- Godoro moja jipya la kitambaa urefu futi 6 na upana futi mbili na nusu (6 kwa $2^1/_2$)
- Shuka mbili zinapatikana shuleni kwa tsh.7,000/= kila moja
- Aje na blanketi moja zito
- Sanduku la bati lenye kufuli imara
- Aje na neti nyeupe ya kuzuia mbu
- Aje na doti moja ya kitenge cha kujifunga wakati wa kuoga tu pamoja na ndala jozi moja **(haruhusiwi kuvaa kitenge wala ndala nje ya bweni)**
- Dawa ya meno, mswaki, mafuta ya kujipaka na sabuni(**Hairuhusiwi kutumia vipodozi vya aina yoyote)**
- Ndoo ndogo mbili za lita kumi kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa na kuogea
- Tochi ya betri au taa ya kutumia mwanga wa jua. (**hairuhusiwi kutuimia taa inayotumia umeme, mafuta ya taa au mshumaa)**

VYOMBO VYA CHAKULA.

- Sahani ya bati (aluminium) yenye sehemu ya mboga ugali na matunda.
- Kikombe kimoja cha bati (aluminium)
- Kijiko
- **Vyombo vya plastiki haviruhusiwi kabisa**

A.VIFAA VYA USAFI

- HGL - Fyekeo(slasher),brashi Ngumu(hardbroom) na ruber squizer
- HGK - Fyekeo(slasher),brashi Ngumu(hardbroom) na brashi dogo la sinki la choo (toilet brush)
- EGM - Fyekeo(slasher),brashi Ngumu(hardbroom)na brashi laini(softbroom)
- HKL –Fyekeo(slasher),brashi Ngumu(hardbroom) na ruber squizer

MUHIMU.

- Kila mwanafunzi aje na sare alizomaliza nazo kidato cha nne.
- Kila mwanafunzi aje na cheti cha kuhitimu kidato cha nne, result slip,cheti cha kuzaliwa pamoja na nakala ya kila cheti.
- Mzazi au mlezi awe tayari kulipa ada na michango mwanzoni mwa muhula ili kuepuka adha ya mtoto kurudishwa nyumbani kwani kutaathiri sana maendeleo ya taaluma yake
- Shule haitoi chakula maalum kwa wanafunzi wenye matatizo ya kiafya kwani chakula cha shule ni kizuri
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula chohote shuleni.
- Mwanafunzi hatakiwi kuchelewa kuripoti kwa tarehe iliyopangwa.
- Mwanafunzi haruhusiwi kupaka rangi kucha, kupaka lipstick, aidha aje amenyoa nywele
- Kwa sare zinazopatikana shuleni mwanafunzi aje na fedha mkononi

B.FOMU 1, na 2,

FOMU 1 ijazwe na mwanafunzi mwenyewe na mzazi au mlezi au Taasisi husika**. FOMU 2** ijazwe na daktari aliyeidhinishwa. Fomu zote 2 zirudishwe shuleni mwanafunzi anapowasili shuleni. Shule ina zahanati inayotoa huduma ya kwanza.Aidha matibabu yanapatikana Hospitali ya Wilaya kwa gharama za mzazi au mlezi hali ikiwa mbaya.

Shule itafunguliwa rasmi tarehe **02/07/2018**. Mwanafunzi atatakiwa afike siku hiyo kabla ya saa 9:30 mchana bila kukosa aje na fomu zote zilizoambatishwa na barua hii zikiwa zimejazwa kikamilifu na wahusika.

MALIPO MBALIMBALI ANAYOPASWA KUJA NAYO

S/N	MAHITAJI	ADA KWA MWAKA 2018/2019	MUHULA WA KWANZA 2018
1.	Ada	70,000/=	35,000/=
2.	Boresha Taaluma	40,000/=	20,000/=
3.	Miundo mbinu	40,000/=	20,000/=
4.	Tiba	20,000/=	10,000/=
5.	Ulinzi	20,000/=	10,000/=
6.	Tahadhari (hairudishwi)	10,000/=	5,000/=
7.	Samani	20,000/=	10,000/=
	JUMLA.	**220,000/=**	**110,000/=**

Aje na Rim ya karatasi nyeupe A4..

Fedha hizi **Zilipwe kwenye akaunti ya shule NMB Tawi lolote Tanzania bara A/C No. 41301100021 Irkisongo Sekondari aje na slip ya benki yenye jina la mwanafunzi sio la mzazi.**

"SIMU ZA MKONONI HAZIRUHUSIWI KABISA KWA MWANAFUNZI"

"ELIMU NI UKOMBOZI"
KARIBU SANA IRKISONGO.

HEADMISTRESS
IRKISONGO SEC SCHOOL

.....

MKUU WA SHULE.

SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI

MWENYEWE KWA HERUFI KUBWA

1. (i) **JINA LA MWANAFUNZI**

……

NB: Jina liwe lile lililotumika kwenye mithani wa KIDATO CHA NNE.

(iii) Tarehe ya kuzaliwa

……Kijiji……Kata…….....

Wilaya

…….....Mkoa……

…….....

2. **JINA LA MZAZI**

(i) Baba mzazi au mlezi……..... .

(ii) Mama mzazi au mlezi …….....

3.KAZI YA:

(i) Baba au mlezi……..Dini…….....dhehebu …….

(ii)Mama au mlezi……Dini…….……..... dhehebu……..

(iii)Anwani ya Mzazi/mlezi……NAMBA YA SIMU ……

(iv) Mwanafunzi anaishi na (weka V sehemu iliyo sahihi)

(a) Baba tu (b) Mama tu (c) Wazazi wote wawili (d) Mlezi (e) shirikani (f) kituo cha malezi

4.MZAZI/MLEZI/ TAASISI ITAYOGHARAMIA MAHITAJI YA SHULE:

(i) Jina …….

(ii) Kazi yake ni …….

(iii)Anuani ya mzazi/Mlezi ……

(iv) Namba yake ya simu……

(v) Uhusiano wake……..Mf. Baba, Mama, Dada, Mjomba au mfadhili .

5. NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

Mimi mzazi/mlezi nadhibitisha kuwa waliojiandikisha hapo chini ni ndugu zangu wa karibu ambao wanaweza kuruhusiwa kumtembelea mtoto wangu na pia shule inaweza kufanya mawasiliano nao kwa masuala yanayomuhusu mwanafunzi huyu.

S/N	MAJINA MATATU	UHUSIANO NA MTOTO	SIMU YA MKONONI	SAINI
1.				
2.				
3.				
4.				

6. UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI:

Mimi …….....nakubali kujiunga na shule ya **IRKISONGO SEKONDARI** na kuthibitisha kuwa, nitafuata sheria na taratibu zote za shule hii ili nitimize lengo la kuja shuleni kwa manufaa yangu binafsi, familia na Taifa kwa ujumla. Endapo nitakwenda kinyume na sheria/kanuni/taratibu za shule nitakubali kuadhibiwa.

Sahihi ya mwanafunzi ……tarehe…….....

7. SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI , MLEZI AU TAASISI HUSIKA

Mimi ……nathibitisha kuwa, taarifa hiyo hapo juu ni sahihi.

Ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule na walimu wote kuhakikisha kijana wangu anakuwa na **NIDHAMU** na **JUHUDI** katika masomo. Aidha, nitagharamia mahitaji yake ya shule, ili kumjengea mazingira mazuri ya kusoma katika kipindi chote atakachokuwa shuleni kwa kuzingatia sheria/kanuni na taratibu za shule.Endapo atafanya uharibifu wowote nitalipa.

Sahihi ya Mzazi /Mlezi/Taasisi……Tarehe……SIMU NAMBA…….....

F2

PRESIDENT`S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

IRKISONGO SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION

To THE MEDICAL OFFICER (GOVERNMENT HOSPITAL)

.....

.....

Please examine the above named student and arrange for any necessary treatment for a student if need be.

HEADMISTRESS
IRKISONGO SEC SCHOOL

.....

THE HEADMISTRESS.

Student's full name:……Age:-……Year.....

REMARKS

SKIN.....

EYES.....

EARS.....

TEETH .....

B/S TEST (CHRONIC).....

PRESURE.....

ABDOMEN.....

CHEST.....

STOMACH.....

URINE.....

HB.HAEMOGLOBIN .....

T.B TEST:-…….....

VDRL.....

HIV TEST:.....

UPT TEST.....

STOOL.....

ULCERS .....

DIABETIC .....

ASTHMATIC .....

Doctors Name..... Signature:……

Designation ……..... Station ……

1. Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Inazingatia miongozo kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na – 25 ya mwaka 1978. Ambayo Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maneno na uje na nakala hii wakati wa kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

iii. Kuhudhuria maandalizi ya jioni na asubuhi (Evening and Morning Preparation)

iv. Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa

v. Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.

vi. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya Shule

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo ndani na nje ya shule.

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kusoma kwa bidii.

2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule

i. Wizi

ii. Uasherati na ushoga,kuchora tatuu,kutumia lugha ya matusi (uhuni na uzinifu)

iii. Ubakaji

iv. Ulevi na matumizi ya madawa yakulevya kama vile uvutaji sigara, bangi,cocaine, mirungi, kuberi

v. Kupigana au kupiga

vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

vii. Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa

viii. kuolewa

ix. Kupata/kutoa mimba

x. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

xi. Kukataa adhabu kwa makusudi

xii. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

xiii. Kuingia nyumba za starehe au nyumba za kulala wageni/guest.